HOTUBA YA MHE. JOHN V.K. MONGELLA, MKUU WA MKOA WA MWANZA KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA WAUGUZI DUNIANI TAREHE 12 MEI, 2017

Mhe. Mary Tesha Onesmo, Mkuu Wa Wilaya ya Nyamagana,

CP Clodwig Mtweve, Katibu Tawala Mkoa wa Mwanza,

Mhe. Christopher Gachuma, Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri Hospitali ya Rufaa ya Mkoa,

Dkt Leonard Subi, Mganga Mkuu Mkoa wa Mwanza,

Dkt Onesmo Rwakyendela, Mganga Mfawidhi Hospitali ya Mkoa,

Viongozi mbalimbali wa Serikali,

Wageni Waalikwa, (Mabibi Na Mabwana)

Wana habari

Awali ya yote, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kutulinda na kutuwezesha kukutana hapa leo. Vilevile nitoe shukrani zangu za dhati kwa uongozi wa chama cha wauguzi Tanzania (TANNA), Tawi la hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mwanza (Sekou toure) kwa kunialika kuwa Mgeni Rasmi katika sherehe hii ya wauguzi duniani yenye malengo ya kumbukumbu ya kuzaliwa mwanzilishi wa huduma za uuguzi duniani hayati **Florence Nightingale** aliyezaliwa tarehe 12/05/1820.

Kutokana na umuhimu wa siku yenyewe ambapo naamini itatukumbusha mengi mazuri aliyofanya Bibi **Florence Nightingale**, nimeona kuna umuhimu wa kushiriki nanyi katika sherehe hii ambayo ni muhimu katika mstakabali wa taaluma ya uuguzi na Taifa letu kwa ujumla. Aidha, natamka wazi kuwa nimefurahia sana kwa nafasi hii mliyonipa ikiwa ni

mara ya kwanza kujumuika nanyi katika sherehe hizi. Pia ikumbukwe kwamba nilipenda sana kupata wasaa ili nipate kuongea nanyi na kuwasikiliza. Asanteni sana.

Ndugu Wauguzi,

Nimeambiwa kuwa, tangu chama cha wauguzi Tanzania kianzishwe, kumekuwa na utaratibu wa kuadhimisha kumbukumbu ya mwanzilishi wa taaluma ya uuguzi duniani kila mwaka.

Ninaamini kuwa kupitia sherehe hii, taaluma ya uuguzi imekuwa ikiboreshwa kwa kufanya tathimini ya utaoaji huduma, na baadhi ya mambo yameendelea kuboreshwa pamoja na kuwepo changamoto nyingi katika taaluma yenu. Leo hii naungana nanyi kwa kusema kuwa, ni muhimu sana sherehe hii iwe inafanyika ili kutukumbusha kufuata maadili na miongozo ya taaluma kama mlivyoachiwa na muasisi wa uuguzi **Florence Nightingale**. Kwa hakika ninawapongeza sana kuandaa sherehe hii.

Ndugu Wauguzi,

Mkumbuke kuwa, sherehe hii inafanyika wakati sekta ya Afya ikiwa katika mkakati wa mageuzi, wenye changamoto nyingi katika kuboresha hali za afya za wananchi kwa kutoa huduma bora.

Rai yangu kwenu, ni kuongeza kasi na ufanisi wa kazi ili kuboresha afya za watanzania. Ninaamini wauguzi ndio jeshi pekee lenye watu wengi walio mstari wa mbele katika sekta ya afya, (takribani asilimia 60 ya watumishi

wote wa afya) ni wauguzi. Kwa mantiki hiyo naamini mna uwezo wa kufikia azma hii, hivyo tuungane na sekta zingine nchini ili taifa liweze kufikia maazimio yaliyokusudiwa kwa kuwaweka watu kwenye afya bora. Na mwisho kuliwezesha taifa la watanzania kutekeleza majukumu yake kiuchumi na maendeleo, kama tunavyoamini kuwa **Afya ni Msingi wa Maendeleo.**

Katika kutekeleza haya yote, najua mengine yako ndani ya uwezo wenu kama wauguzi na wanachama, na mengine ni ya uongozi mahali pa kazi na serikali kwa ujumla. Serikali yetu inajitahidi iwezavyo kuboresha hali ya afya za wananchi wake na kuwajengea uwezo wale wote wanaohusika katika kuwahudumia wananchi.

Ndugu Wauguzi,

Serikali inatambua umuhimu wa wauguzi katika sekta ya Afya. Ninapenda niupongeze uongozi wa Chama cha Wauguzi Tanzania (TANNA) pamoja na wauguzi wote kwa kujitoa kwa moyo wa dhati pamoja na kuwa na changamoto mbalimbali mnazokabiliana nazo katika utoaji huduma.

Aidha,ninawapongeza sana kwa huduma za jamii mliozota kwenye mabanda ya maonesho mmeonesha umahili mkubwa katika huduma zenu pia,zawadi mlizotoa kwa wagonjwa, ambapo mmeonyesha upendo aliokuwa nao mwanzilishi wa taaluma ya uuguzi duniani.

Hata hivyo, napenda kuwafahamisha kuwa, serikali imekuwa ikiendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi wake kadri ya uwezo unavyoruhusu. Ninawaomba wauguzi wote Mkoa wa Mwanza kuwa na subira, pia kutoa ushirikiano wakati serikali ikiendelea kushughulikia suala hili la uboreshaji pamoja na hoja nyingine mlizokwisha ziwasilisha.

Ndugu Wauguzi,

Ni jambo la pekee kwa wauguzi katika sherehe hii mwaka huu, kutathmini wajibu wenu wa kuwahudumia wananchi na kuziangalia changamoto zinazotokana na wajibu huo. Wote tunajua mikakati iliyoko mbele yetu ya kuwahudumia wananchi pamoja na watoa huduma katika awamu hii ya tano.

Nimefurahi kusikia kauli mbiu yenu ya mwaka huu 2017 inayosema

"NURSES – A VOICE TO LEAD ACHIEVING SUSTAINABLE DEVELOPMENT GOAL"

(WAUGUZI: MBIU YA KUYAFIKIA MALENGO ENDELEVU YA MILLENIA).

Kwa sababu bado mna ushirikiano mzuri ninyi kwa ninyi kwa wagonjwa na wateja na hata taasisi zingine zinazotoa huduma mbalimbali katika jamii yetu.

Ndugu wauguzi,

Natambua kuwa mnafanya kazi kwa juhudi na kufuata taratibu za kazi, niwaombe mwendelee na moyo huo, japokuwa changamoto haziwezi kukosa. Wauguzi mnao mtazamo mpana sana pindi mgonjwa anapokuja kutibiwa kwa kutambua shida na mahitaji ya mgonjwa kwa nyakati mbali mbali na kutoa huduma kulingana na shida au hitaji la mgonjwa huyo.

Ndugu Wauguzi,

Ningependa kuwapongeza kwa mara nyingine, kwa jinsi mnavyofanya kazi katika mazingira magumu kama changamoto zenu zilivyoainishwa. Serikali inatambua kwamba kwa muda mrefu huduma za afya zimekuwa zikikabiriwa na uhaba wa vitendea kazi na rasilimali watu ukilinganisha na mahitaji ya wananchi. Hatua mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa ili kuhakikisha utendaji kazi unakuwa rahisi zaidi kwa kuwa na vitendea kazi vinavyokidhi huduma za msingi na zilizo bora.

Tatizo sugu la usafiri ambalo limekuwa likiwasumbua muda mrefu, ofisi yangu itaendelea kulifanyia kazi na nitaomba Mkurugenzi wa Jiji na Sumatra tukae pamoja ili tuone jinsi ya kulitatua haraka iwezekanavyo.

Pamoja na hayo yote ambayo serikali inajitahidi kuyafanya, natambua kuwa safari bado ni ndefu, lakini jitihada zitaendela kufanyika ili

kuhakikisha huduma zinatolewa kwa kiwango cha kuridhisha. Pia niwaombe kuzingatie maadili ya kazi ikiwemo kuwahi kazini, kuvaa sare au nguo zenye nidhamu ndani na nje ya kazi, kutumia lugha nzuri kwa wateja na wagonjwa wetu na mengine mengi yanayohusu kanuni na sheria na taratibu za utumishi.

Mwisho.

Naomba kuwashukuru tena wote mliofika hapa, matumaini yangu ni kwamba tutazidi kuwa pamoja kwa mara nyingine katika sherehe zenu na kazi zenu za kila siku.

Baada ya kusema hayo sasa napenda kuwatakia sherehe njema na kazi njema.
Mungu awabariki sana.

"Asanteni kwa kunisikiliza".